**Mwelekeo wa Ubinafsishaji wa Maji hatimaye Wageuka?**

Nick Buxton <http://www.tni.org/users/nick-buxton>
Septemba 2010

Tangazo la Jumuiya ya Ulaya ya kutoa kiasi cha euro milioni 40 kusaidia “wabia wasiotoa huduma zao za maji safi na taka kwa faida” katika Afrika, Caribbean na Pacific ni uthibitisho wa karibuni kuwa msukumo wa uongozi wa ubinafsishaji wa maji umelazimishwa kurudi nyuma.

Kuna picha ya vita vya maji vya Bolivia ambayo kwa ujumla ni kielelezo cha ushujaa wa kijasiri katika kupinga mapambano ndani ya mraba wa Tiannmen.

Inaonyesha mwanamke mwasilia na wa kipekee, aliyesuka nywele na sketi yenye mikunjo, anayeashiria manati dhidi ya mstari wa kipolisi usiotulizika.

Inaashiria uhodari wa upinzani wa watu wa Cochabamba waliofanikiwa mwezi Aprili 2000 katika kuiondoa kampuni ya kimataifa ya Bechtel ya California ambayo ilibinafsisha maji yao na kusababisha viwango vya gharama za huduma kupaa.

Pamoja na haya, pia inaonyesha hisia dhidi ya nguvu ya miundo kandamizi ambayo ni miongoni mwa vikwazo vinavyokabiliana na ubinafsishaji wa maji.

Kwa mwaka 2000 kiwango cha juu cha wimbi la ubinafsishaji wa maji katika nchi zinazoendelea kilirikodiwa, wakati kwa ujumla taasisi karibu zote kutoka Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) zilihoji kuwa ni sekta binafsi tu zinaweza kuleta matumaini ya kupatikana maji safi kwa kila mtu.

Kuchukizwa kwa Cochabamba kuliungwa mkono na vyama vya kijamii kwa sababu ilikuwa kikwazo cha awali katika kukabili wimbi lisilozuilika kuhusu ubinafsishaji.

Miaka kumi baada ya Vita vya Maji, pamoja na kutambua faida zilizotokea, imeendelea kuonekana kama vita vya maji vya Bolivia si kuwa tu ni kielelezo cha kishujaa, bali pia kama mwanzo wa mageuzi ya ubinafsishaji wa maji.

*kurudi nyuma kwa ubinafsishaji*

Mwanzoni mwa mwaka huu, Paris iligeuza ubinafsishaji wa maji na kuweka mikononi mwa mamlaka ya mabaraza ya Manispaa.

Hii imekuwa kama kigezo makini na kikubwa cha ubinafsishaji wa maji barani Ulaya kwenye makao makuu ya Ufaransa. Katika mwezi wa August, Bolivia ilifanikiwa kuweka msukumo kupitia azimio la Umoja wa Mataifa linalounga mkono kuwa maji ni haki ya kibinadamu, ambalo wakati halizuii ubinafsishaji, lakini linaweka msisitizo juu ya maji kama haki ya kibinadamu kuliko kuwa chanzo cha kujipatia faida.

Hatimaye, ushahidi wa mwisho ulijitokeza majira ya kiangazi, kwa Jumuiya ya Ulaya kutangaza mpango mpya wa euro milioni 40 kusaidia wabia wake wa maji safi na taka katika Afrika, Carribean na Pacific.

Olivier Hoedeman, mtafiti wa siku nyingi na mwanaharakati wa masuala ya maji na mjumbe wa TNI na mshirika wa mradi wa kituo cha masuala ya uchunguzi wa masuala ya haki za maji kuhusu umuhimu wa Mfuko mpya wa wabia wa maji wa ACP-EU, "Mfuko huu unaonekana kutokuwa na madhara, lakini kwa uhakika unaonyesha tofauti kubwa na sera ya maji ya Jumuiya ya Ulaya".

Kwa miaka kumi, mfumo wa Jumuiya ya Ulaya ulitawaliwa na imani kwamba kuihusisha sekta binafsi ndio pekee ungeweza kuleta ubora wa sekta ya maji kwa nchi zinazoendelea.

Sekta ya umma ilipuuzwa kabisa na kutazamwa kama mtindo wa kizamani, uliopitwa na wakati na usiokubalika, hata kama sekta ya umma iliendelea kutawala usambazaji wa maji na taka duniani.

Kabla ya 2020, mtazamo wa ndani wa Jumuiya ya Ulaya kuhusu maji ulikuwa ni kielelezo katika kuzindua mpango wa maji mwaka 2003, ambao kwa bayana ulielezea kusudio lake la kupanua uwajibikaji wa sekta binafsi kujihusisha na maji, hususan kusaidia kampuni binafsi za maji kuenea katika nchi zinazoendelea.

Kamishina wa maji wa Jumuiya ya Ulaya Louis Michel aliunga mkono itikadi hii kwa kuwekeza euro milioni moja kwa mwaka katika mpango wa huduma za ushauri wa miundombinu wa sekta za umma na binafsi (PPIAF) pamoja na Ulaya kuweka mizania ya usawa ambapo Mpango wa Uwezeshaji wa Sekta Binafsi wa Mazingira (PSEEF) ulitenga bajeti ya euro milioni 20. Katika ngazi ya Taifa, wanachama wengi wa Ulaya walitoa misaada yenye masharti kwa miradi ya maji katika kushirikisha sekta binafsi

*Kugeuka kwa Jumuiya ya Ulaya*

Tofauti na picha hii, kuweka mpango hususan kusaidia ubia usio wa uzalishaji wa faida ulikuwa ni mwelekeo mpya na unaopeleka mbele umuhimu wake. Emanuele Lobina, mtafiti wa Kitengo cha Kimataifa cha Huduma za Umma (PSIRU) kilichoko katika Chuo Kikuu cha Greenwich, London husema; "Hii ni mara ya kwanza kwa wafadhili wakubwa kama Jumuiya ya Ulaya kuvumisha umuhimu wa dhati wa kuongeza utoaji wa fedha kusaidia kujenga uwezo wa maendeleo ya sekta ya maji kwa eneo husika.

Mkazo wake katika kusaidia wabia wasio zalisha faida una maana kuwa rasilimali za fedha na watu zilizopo zilizokusudiwa kujenga uwezo wa kimaendeleo katika sekta ya maji safi na taka katika ACP hazitaweza kuchepua manufaa ya kibiashara.

Lobina anasema pia kuwa fedha ingeweza kuwa na umuhimu wa kuchochea athari. "Kiwango cha juu cha ruzuku ni euro milioni moja na cha chini ni euro 250,000 hivyo kuna nguvu kubwa ya kujenga ubia ambao ulikuwa haupo hapo awali.

Wakati tulipochambua hali ya ubia wa Umma - Umma (PUPs) mwaka 2009, tulipata idadi ya zaidi ya 130 katika nchi karibu 70, ambapo ni kiwango cha juu zaidi ya kile cha Umma – Binafsi (PPPs) katika sekta ya maji licha ya misaada ya ufadhili wa jamii kwa PPPs. Kwa hiyo ilionekana umuhimu wa uwezekano wa kuongeza makumi ya ubia mpya na wa wazi wa Umma – Umma kama matokeo ya mpango huu.

*Gharama za ubinafsishaji kwa kifupi; uchambuzi mbadala**

Olivier Hoedeman anaeleza sababu ya Ulaya kubadilisha mwelekeo katika kutoa misaada kwa Ubia wa Maji wa Umma – Umma kwa njia tatu. Kwanza Umoja wa Ulaya ulilazimishwa kutambua kushindwa kwa ubinafsishaji kwa kuwa kuna aina nyingi ya miradi ya ubinafsishaji wa maji katika nchi zinazoendelea ambazo zilianguka wakati makampuni ya maji yalipojitoa au yalipolazimishwa kujiondoa kutokana na msukumo wa maandamano ya nguvu ya umma.

“Ni wazi kuwa sekta binafsi ama haikuwa na uwezo au haikutaka kupanua huduma za maji kwa jamii maskini. Ukweli uliokuwepo kwa urahisi uliibua ahadi za uongo za ubinafsishaji zinazotetewa”.

Alhassan Adam, mwanaharakati wa maji kutoka Ghana anasema katika miaka hii ya karibuni, “Mpango wa uwekezaji wa maji wa sekta binafsi unaanguka vibaya katika Afrika. Wote waliochukua hatua za hatari kuhusu maji wanajiondoa kutokana na mapato duni na mifulilizo ya kampeni zinazofanywa na raia.

Pili, taasisi kama Tume ya Ulaya iliendelea kukabiliana na shinikizo kutoka kwa vyama vya kiraia, ikiwa ni pamoja na tafiti makini juu ya udhaifu wa taarifa kuhusu ubinafsishaji wa maji na pia upinzani wa umma unaojitokeza katika miradi mingi ya ubinafsishaji wa maji, hususan katika Afrika. Kidunia, na hata kwenye mabaraza shirikishi yanayotawala kama vile Baraza la Maji la Dunia, ambayo ni sauti dhidi ya ubinafsishaji imekuwa ni mifumo inayosikika na isiyostahili kupuuzwa kamwe.

<http://www.nytimes.com/2006/03/20/international/americas/20water.html>

Hapa nyumbani, Jumuiya ya Ulaya isingeweza kupuuzia uhamasishaji unaotokea Brussels dhidi ya ubinafsishaji wa maji. Hoedeman anarejea mfano mmoja kuhusu maandamano makubwa siku ya maji Duniani mwaka 2006 ambayo yaliwaleta wanaharakati wa maji na vyama vya wafanyakazi pamoja, na yaliunganisha Makao Makuu ya kamisheni na Aquafed, muungano wa washirika wa mipango ya maji.

“Ilikuwa vigumu sana kwa Kamisheni ya Ulaya kutetea mfumo wake hususan wakati hata Ofisi ya ukaguzi wa Kamisheni ya Ulaya ilionyesha kwamba Jumuiya ya Ulaya inasisitiza juu ya udhaifu na matumizi mabaya ya fedha za walipakodi unaotokana na Ubia wa Umma na Binafsi”

Tatu, vikundi vingi vinavyopinga ubinafsishaji katika miaka ya karibuni imeelekeza rasilimali nyingi katika juhudi mbadala na kuchambua jinsi maeneo hayo yanavyoweza kupewa kipaumbele. Nyingi ya chunguzi kifani zilikusanywa na kuwekwa katika kitabu kwenye mtandao, /Kudai Maji kwa Umma – Mafanikio, Mapambano na Dira kutoka pande zote za Dunia <http://www.tni.org/tnibook/reclaiming-public-water-2>/,

Uchapishaji wa pamoja ulifanywa na TNI na Kituo cha Ulaya cha mwenendo wa anga, Kituo cha huduma za umma cha utafiti cha kimataifa (PSIRU) pia kimekuwa na machapisho mengi kuhusu uboreshaji wa menejimenti ya umma ya maji na Ubia wa Umma-Umma ambao umetoa utafiti wa manufaa sana ambao mpaka sasa hayajawekwa pamoja.

“Tunafahamu kwa ushahidi wa maneno, kuwa maafisa wa EU walizipata ripoti hizi kwa njia ya intaneti, wakati muungano wa upinzani wa vyama vya Kijamii na kushindwa kwa miradi ya ubinafsishaji ililazimisha Kamisheni ya Ulaya kuangalia njia mbadala”, anasema Hoedeman.

*Mapambano yanaendelea*
Hoedeman anaonya kwa kusema kuwa mapambano dhidi ya ubinafsishaji wa maji hayajafanikiwa bado. “kuna sababu za kutokujipongeza kwa sauti.Tunajua kulikuwa na mvutano hata kuhusu kufadhili mpango huu, kwa serikali za Ufaransa na Uingereza, na kuwa bado kuna mpasuko ndani ya kamisheni. Bado kuna itikadi pinzani za kina ndani ya EU kuhusiana na mifumo hii. Mapambano ni budi yaendelee. Sisi kwa bahati mbaya hatuwezi kupunguza kasi au kufikiri kuwa mambo yataendelea kwa mwelekeo huu”.

Kwa mujibu wa tangazo la Shirika la Fedha la Kimataifa la Benki ya dunia la mwezi Septemba, euro milioni 100 zilizotolewa kwa Veolia Voda kupanua huduma za ubinafsishaji wa maji ulaya Mashariki inathibitisha hili. Alhassan Adam pia anaonya kuwa bado tuna njia ya kufanya kuzishawishi taasisi na serkali kuhusu ukweli “kwamba sekta binafsi ni dhaifu na inayotegemea fedha za umma kwa ajili ya kuwekeza na kwamba sekta binafsi haina nia kwa watu wasio na uwezo kifedha wa kulipia huduma zao”.

Hata hivyo, Hoedeman na Alhassan wana matumaini kuhusu jitihada hizi. Hoedeman anatoa maoni: “Naamini uwekezaji huu unaweza kuonyesha uwezo wa kweli wa ubia wa umma-umma na kuweka cheche kupata mabadiliko makubwa zaidi.

Muhimu sasa ni kupanua kwanza kwa kanda nyingine, na kusukuma mfumo kama huo kwa taasisi nyingine”. Alhassan Adam anaamini kuwa ingewezekana kuhamasisha kuinua sekta ya umma: “Kusaidia ubia wa umma-umma unaweza kuimarisha kupandisha hamasa ambayo ilikuwa imeshuka baada ya wimbi la ubinafsishaji miaka ya 1990. Hii ingeenda sambamba na udhibiti wa rasilimali ya Taifa, haki miliki na maridhiano.

Labda muhimu zaidi, ari iliyoonyeshwa inatoa mfano mzuri kuhusu nini kinaweza kufikiwa kama vyama vya kiraia vingeweka nguvu ya pamoja, inayojumuisha nguvu za ziada na mbadala zilizojitokeza.

Uzoefu huu hususan kwa sasa ambapo serikali nyingi hutumia migogoro ya kifedha kudhoofisha umuhimu wa huduma za umma. Hoedeman anaamini kuwa mafunzo yaliyotokana na mwenendo wa ubinafsishaji wa maji lazima uzingatie wote wanaotetea huduma za umma: “Tunatambua kuwa hii ni hatua moja katika safari ndefu ya mapambano ambayo itazingatia sasa umuhimu wa kutetea huduma zote za umma. Lakini, hii haitoshi kujitetea na kupinga tu. Njia pekee ni kutetea na kuongeza kasi ya kuwekeza kwenye huduma za umma ili ziwe ni huduma zinazolinda na kujenga watu.

*Kwa Mashirika yenye Nia*
/Emanuele Lobina anaalika mashirika ya kiraia na vyama vya wafanyakazi kutia moyo waombaji wenye nguvu na wabia ikiwa ni pamoja na Maji Safi na Taka, Mamlaka ya

Mitaa na Mashirika mengine ya maji katika nchi za ACP na Jumuiya ya Ulaya (EU), kutuma muhtasari wa dhana (usiozidi kurasa 4) kabla ya 6 Oktoba 2010. Kwa maelezo na ushauri zaidi, pamoja na huduma kuhusu upatikanaji wa fedha, jisajili http://www.acp-eu-waterpartnerships.org <http://www.acp-eu-waterpartnerships.org/> tovuti na mawasiliano e.lobina@gre.ac.uk <barua: e.lobina@gre.ac.uk> au piga (+442083318476)/

Nick Buxton <http://www.tni.org/users/nick-buxton>

Mawasiliano kwa intaneti na afisa habari

Kwa mawasiliano ya intaneti na afisa habari

Nick Buxton ni mshauri wa mawasiliano anayeshughulikia habari, machapisho na mawasiliano ya intaneti TNI. Anakaa California tangu Septemba 2008 na awali akiishi Bolivia kwa miaka minne, akifanya kazi kama mwandishi/mhariri wa tovuti, Fundación Solón <http://www.funsolon.org/>, shirika la Bolivia akishughulikia masuala ya biashara, maji, utamaduni na kumbukumbu.

Yeye ni mwanaharakati wa muda mrefu wa masuala ya Kidunia ya haki na amani. Mwishoni mwa 1990 alikuwa meneja wa mawasiliano wa Jubilee 2000, ambayo ni sehemu ya harakati za Kidunia juu ya Madeni Batili ya Kimataifa na kuyaweka katika ajenda za Kisiasa Duniani.

Machapisho yake yanahusisha "Mtandao wa Uondoaji wa Madeni" katika utetezi, uanaharakati na intaneti / (Lyceum books, 2001); Vyama vya kiraia na uondoaji wa madeni" katika/Vyama vya kiraia na haki za binadamu/ (Routledge, 2004) na "Siasa za madeni" katika /Utu na Ujasiri; changamoto za utandawazi Bolivia/Chuo kikuu cha California Press/Merlin Press UK, Januari 2009).